



CHAMA CHA WAHASIBU TANZANIA (TAA)

TAARIFA KWA WANACHAMA KUHUSU MKUTANO MKUU WA 43 WA MWAKA 2026

Kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), Sehemu ya 11, Ibara ya 3, Rais wa Chama cha Wahasibu Tanzania anapenda kuwajulisha wanachama wote kuwa **Mkutano Mkuu wa 43 wa Mwaka (Annual General Meeting – AGM)** utafanyika tarehe **17 Oktoba 2026**, kuanzia **saa 2:30 asubuhi, jijini Dar es Salaam**.

USHIRIKI KATIKA MKUTANO

Wanachama wote wanakaribishwa kushiriki katika Mkutano Mkuu huu bila malipo. Hakutakuwa na ada yoyote itakayolipwa na mwanachama kwa ajili ya kushiriki katika mkutano huu.

Mkutano Mkuu utakuwa na sehemu kuu mbili. Katika sehemu ya kwanza, ambayo itafanyika asubuhi, wanachama watapata **mafunzo maalum kuhusu stadi za kazi na maisha (Soft Skills)**. Baada ya mafunzo hayo, sehemu ya pili itahusisha mkutano rasmi ambapo wanachama watapata fursa ya kupokea taarifa, kujadili masuala mbalimbali na kutoa maoni kuhusu maendeleo ya Chama.

MASUALA YATAKAYOWASILISHWA NA KUJADILIWA

Miongoni mwa masuala yatakayowasilishwa na kujadiliwa katika Mkutano Mkuu ni:

1. Kupokea na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Baraza la Uongozi kuhusu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chama kwa mwaka 2025/2026.
2. Kupokea na kujadili Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa mwaka wa fedha 2025/2026.
3. Kupokea na kujadili Bajeti ya Chama kwa mwaka wa fedha 2026/2027.
4. Kupokea na kujadili Mpango wa Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chama kwa mwaka 2026/2027.
5. Kujadili na kupitisha marekebisho ya Katiba ya Chama, pale yatakapopendekezwa.
6. Kufanya Uchaguzi Mkuu wa Viongozi wa Chama kwa nafasi zifuatazo:
 - Rais;
 - Makamu wa Rais; na
 - Wajumbe wa Baraza la Uongozi.

Kumbuka: Ni wanachama walio hai na wanaokidhi masharti yaliyowekwa na Katiba ya Chama pekee watakaokuwa na haki ya kupiga kura, kuchagua na kuchaguliwa.

7. Mengineyo, kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

MASAA YA MAFUNZO ENDELEVU YA KITAALUMA (CPD)

Wanachama watakaoshiriki katika Mkutano Mkuu watapata masaa ya Mafunzo Endelevu ya Kitaaluma (Continuing Professional Development – CPD) kwa mujibu wa taratibu husika.

Ili kuthibitisha ushiriki, link maalum ya usajili itatumwa kwa wanachama wote. Wanachama wanashauriwa kujisajili mapema ili kuwezesha maandalizi ya mkutano na uthibitisho wa ushiriki.

ENEO LA MKUTANO

Eneo ambalo Mkutano Mkuu utafanyika litatangazwa baadaye kupitia njia rasmi za mawasiliano za Chama.

Wanachama wote wanahimizwa kutenga muda na kushiriki kikamilifu katika Mkutano Mkuu huu, ambao ni fursa muhimu ya kujadili maendeleo ya Chama, kutoa maoni na kushiriki katika kufanya maamuzi kuhusu masuala muhimu ya Chama.

Ushiriki Wako Ni Muhimu Katika Kujenga Chama Imara, Cha Kisasa Na Chenye Ubora Wa Kitaaluma.

Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA)

27 Agosti 2026 | Dar es Salaam

